



Ni sunna kwa imam na mwenye kuswali peke yake aswali kuelekea sutra. Na sutra ya imaam ni sutra ya aliye nyuma yake.




Na atajaalia macho yake sehemu anayosujudia, wala asigeuke geuke.



Na atajaalia umbali wa nyayo ylzake kama umbali wa mabega yake hatozidisha wala kupunguza na ataweka sawa miguu yake.







Baada ya kuleta sharti za swala atasema "Allaahu akbar" pamoja na kunyanyua mikono hali ya kubandanisha vidole usawa wa masikio au mabega na atajaalia ndani ya viganja kuelekea qibla.



3

Kisha ataeka kiganja chake cha kulia juu ya nje ya kiganja na mkono wa kushoto juu ya kifua chake.



4

Kisha ni sunna kusoma dua ya kufungulia swala katikavrakaa ya kwanza tu na ni bora afanye aina tifaute tofauti za kufungulia swala na atasema "Subhaanaka Allaahumma wa bihamdik wa tabaaraka ismuk wa ta'ala jadduka wa laa ilaaha ghayruk.

Kisha atasema "A'uudhu billaahi mi shaytwaani rrajiim"

Kisha Atasoma bismillaahi na atasoma suratul faatiha kama ilivyopangiliwa kwa aya zake na maneno yake na herufi zake na haraka zake.





Bismillahi rrahmani rrahiim(1)

Alhamdu lillaahi rabbil aalaamiin (2) Arrahmaani rrahiim (3) Maaliki yawmi ddiin (4) Iyyaaka na'budu wa iyyaaka nasta'iin (5) Ihdina sswiraatwa lmustaqiim (6) swiraatwa lladhiina an'ama 'alayhim ghayril maghdhwuubi 'alayhim wala dhwaalliin (7)

Kisha atasoma kinamwepesikia katika Qur'an (sunna) bila ya kuleta isti'aadha na atasoma bismillaahi mwanzi wa sura tu.

5

Kisha atanyanyua mikono yake kama alivyonyanyua katika takbira ya kuhirimia swala hali ya kusema "Allaahu akbar" na atarukuu kisha atakamata magoti yake na wala hatokunja viwiko vyake na atafanya mgongo wake kuwa sawa na kichwa chake na atasema mara moja kwa uwajibu "subhaana rabbiyal 'adhwiiim" na ni sunna kuzidisha kwa yaliyothibiti.




6

Kisha wakati wa kunyanyuka na kabla ya i'tidaal atasema "sami'a Llaahu liman hamidah" pamoja na kunyanyua mikono yake usawa wa masikio yake au mabega yake.

Atakaponyooka wima atasema "Rabbanaa wa laka lhamd" na ni sunna kuzidisha dua zilizothihiti


Kisha ataleta takbira bila ya kunyanyua mikono na atasujudu juu ya viungo saba : paji la uso, pua na viganja viwili na magoti mawili na matumbo ya vidole vya miguu.

Na ataweka umbali baina ya makwapa na baina ya tumbo na mapaja na baina ya mapaja na miundi navatanyanyua dhiraazake.







7

Na atasema "subhaana rabbiyal a'laa" mara moja wajibu na atazidisha kwa zilizothibiti katika adhkaar na inafaa aombe anachotaka na bora aombe kwa dua zilizothibiti.




8

Kisha atatoa takbira na atakalia mguu wake wa kushoto hali ya kuwa ameutandaza na ataunyanaya wa kulia na ataweka matumbo ya vidole vya kulia ardhini na vidole vyake kuelekea qibla, na ataweka viganja vyake kuu ya mapaja yake na atasema "Rabbi ghfirliiy". Hiki kikazi ni katika vikazo vyite vya swala isipokuwa katika swala ya rakaa 3 na 4 katika tashahhud ya mwisho atakaa "tawarruk" kwa kufanya mguu wake wa kushoto chini ya muundi wa kulia.




9

Kisha atatoa takbira na atasujudu kama sijda ya kwanza kisha atatoa takbira na atasimama kwa ajili ya rakaa ya pili na atafanya kama alivyofanya katika rakaa ya kwanza isipokuwa katika rakaa ya pili hakuna takbira ya kuhirimia na dua ya kufungulia swala.



Atakapomaliza sijda ya pili atakaa kwa ajili ya tashahhud.



Na ataashiria kwa kidole chake cha ishara na atazungusha duara kidole cha kati na gumba, na atatikisa kidole cha ishara na kuomba.




Na atasoma tashahhud kisha swalaatul ibraahimiyya "Attahiyyaatu lillahi waswalawatu wa twayyibaatu assalaamu 'alayka ayyuha nnabiyyu warahmatullah wabarakaatuh assalaamu 'alaynaa wa 'alaa 'ibaadi llaahi swaalihiin ash hadu an la ilaaha illa llah wa ash hadu anna muhammadan 'abduhu warasuuluh Allahumma swalli alaa muhammad wa 'alaa aali muhammad kama swallayta 'alaa ibrahim wa 'alaa aali ibrahim innaka hamiidun majiid Allaahumma baarik alaa muhammad wa 'alaa aali muhammad kama baarakta 'alaa ibrahim wa 'alaa aali ibrahim innaka hamiidun majiid.

Kisha ataomba kinga kutokana na mambo manne "Allaahumma inni a'udhubika min 'adhaabi jahannam wa a'udhubika min 'adhaabil qabr wa a'udhubika min fitnatil mahyaavwal mamaat" na ataomba anachokitaka na bora aombe kwa yale yaliyothibiti pamoja na kusema "Allaahumma a'inni 'alaa dhikrika wa shukrika wa hisni 'ibaadatik"

Kisha atatoa salamu mbili kulia na kushotoni kwake hali ya kusema "Assalaamu 'alaykum wawrahmatullaah" na atageuka kwa kichwa chake tu bila ya mabega na bila ya kutikisa kichwa juu na chini na bila ya kuashiria kwa mikono .



10



10

Ameweka taaliki Sheikh Dktuur Haytham Sarhaan , Mwalim wa zamani masjid annabawiy

Na msimamizi wa maahad ya sunna : mahadusunnah.com

Haki za kuchapa na kusambaza zipo huru.
Tarjama ya kipeperushi «sarhaan.com» Au pangusa bar code

